SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Jarida la

# RELI NA MATUKIO

Toleo namba 37, Juni - Agosti 2024

Habari | Makala | Matukio | Elimu | Picha




# DKT. SAMIA AANDIKA HISTORIA UZINDUZI WA SGR NCHINI

Na Mwandishi wetu.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amezindua rasmi huduma za safari za treni za abiria katika reli ya kiwango cha kimataifa - SGR, miundombinu ya reli na stasheni kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma, hafla ya uzinduzi imefanyika katika Stesheni ya SGR mkoani Dodoma Agosti 1, 2024.

Mhe. Rais amesema Serikali imewekeza takriban dola za kimarekani billioni 10 sawa na Shilingi trilioni 23.3 katika mradi wa SGR kwa lengo la kuboresha ustawi wa maendeleo ya wananchi kwa kasi na kupunguza gharama na muda za usafirishaji wa mizigo na abiria kutoka saa 9 hadi saa 3:30 kwa safari ya kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma.

Inaendelea Uk. 2

## RAIS WA GUINEA BISSAU ATEMBELEA TRC NA KUJIONEA SHUGHULI ZA USAFIRISHAJI WA TRENI ZA SGR Uk. 4



Rais wa Jamhuri ya Guinea Bissau Mhe. Umaro Sissoco Embalo (aliyevaa tai ya bluu) akiwa katika treni alipotembelea Shirika la Reli Tanzania - TRC kujionea Ujenzi wa Reli ya Kiwango cha Kimataifa - SGR hivi karibuni, 2024.

# DKT. SAMIA AANDIKA HISTORIA UZINDUZI WA SGR NCHINI



Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwaaga baadhi ya abiria waliokuwa ndani ya treni ya kisasa mara baada ya kuzindua miundombinu ya reli ya kiwango cha kimataifa - SGR na huduma za treni za SGR kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma Agosti 1, 2024



Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan (kulia), Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndani ya treni akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa kuhusu huduma za usafiri wa treni za mwendokasi kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma Agosti 1, 2024

**Inatoka Uk. 01**

Mhe. Rais amesema maendeleo ni hatua kwasababu ujenzi wa reli hii ya kiwango cha kimataifa ilianza kwa maongezi kwa viongozi wa Afrika Mashariki katika Serikali ya awamu ya tatu chini ya uongozi wa hayati Benjamin Mkapa, Serikali ya awamu ya nne chini ya Mhe. Jakaya Kikwete ilifanya upembuzi yakinifu, Serikali ya awamu ya tano chini ya uongozi wa hayati John Magufuli ilianza ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa na sasa Serikali ya awamu ya sita inaendeleza mradi huu kwa falsafa ya kazi iendelee

"Reli hii ina faida nyingi italinda mazingira, itaongeza ajira, itapunguza msongamano wa magari na itaongeza ufanisi wa bandari kwasababu ya uwezo wa kubeba mzigo mwingi kwa wakati mmoja" alisema Mhe. Rais

Mhe. Rais ameipongeza Wizara ya Uchukuzi, Shirika la Reli Tanzania pamoja na wadau wote kwa usimamizi makini wa mradi huu wa kimkakati wa reli ya kiwango cha kimataifa ambao unabeba sura na ndoto kubwa ya taifa.

Mhe. Rais ametoa wito kwa Wizara ya Uchukuzi, Shirika la Reli Tanzania, wasimamizi pamoja na wakandarasi kuhakikisha mradi huu unakamilika kwa wakati na kwa viwango vya kimataifa

"Napenda kuwaasa wananchi wenzangu kuwa reli hii ya SGR ni tunu muhimu kwa uchumi wetu tuihifadhi, tuithamini na kuipenda" alisema Mhe. Rais

Mhe. Rais ameridhia ombi la Mkurugenzi Mkuu wa Shrlirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kadogosa Stesheni ya SGR Dodoma iitwe Samia Suluhu Hassan na kutoa majina kwa stesheni za SGR Morogoro kuitwa Jakaya Kikwete, stesheni ya Dar es Salaam kuitwa John Magufuli, stasheni ya Tabora kuitwa Ally Hassan Mwinyi stesheni ya Shinyanga kuitwa Abed Karume, stesheni ya Mwanza kuitwa Julius Nyerere na stesheni ya Kigoma kuitwa Benjamin Mkapa.

Waziri wa Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa amesema Serikali ya awamu ya sita imekamilisha reli ya kiwango cha kimataifa kwa kilometa 722 ambazo tunazizindua leo na imeanzisha vipande vingine vya ujenzi wa SGR kwa kilometa 1560 na kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza barani Afrika kuwa na reli ndefu ya SGR inayotumia nishati umeme.

Mkurugenzi mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kadogosa amesema Shirika limenunua vitendea kazi mbalimbali ikiwemo vichwa 19 vya treni ya umeme, mabehewa 89, treni za kisasa EMU seti 10 na mabehewa ya mizigo 1430 thamani ya uwekezaji huu ni wa Shilingi trilion 1.8, aidha Kadogosa ameeleza kwa kusema Shirika limeshapokea vichwa 17 vya SGR mabehewa 65 na seti 3 za treni ya kisasa EMU.

**Inaendelea uk. 3**



Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhe. Husein Ally Mwinyi (wa pili kulia) akiwasili katika stesheni ya SGR ya Magufuli jijini Dar es Salaam kwaajili ya  hafla ya uzinduzi wa huduma za treni za mwendokasi na miundombinu ya reli ya kiwango cha kimataifa - SGR Dar es Salaam hadi Dodoma Agosti, 2024.

# DKT. SAMIA AANDIKA HISTORIA UZINDUZI WA SGR NCHINI

Inatoka Uk. 2

"Ulipoingia madarakani Mhe. Rais uliahidi utaendeleza ujenzi wa reli ya SGR na leo tunashuhudia ukamilishwaji na kuanza safari za abiria kati ya Dar es Salaam na Dodoma na maendeleo ya ujenzi wa vipande vingine vya reli ya kiwango cha kimataifa SGR" alisema Kadogosa

Treni ya SGR Tanzania imesanifiwa kwa viwango vya kimataifa na kuifanya Tanzania kupata tuzo mbili za kimataifa. Tangu kuanza usafirishaji wa abiria kwa treni ya kiwango cha kimataifa tarehe 14 Juni 2024 imeshasafirisha abiria laki moja na elfu themanini na nane (188,000) hii ni sawa na wastani wa abiria elfu saba (7,000) kwa siku. Safari za abiria kwa treni ya kiwango cha kimataifa zinaendelea kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro na Dar es Salaam hadi Dodoma




Rais wa Jamhuri ya Muunganowa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan (kati) akikata utepe kuashiria uzinduzi wa huduma za usafiri wa treni za mwendokasi katika stesheni ya Magufuli jijini Dar es Salaam, Agosti 2024.



Rais wa Jamhuri ya Muunganowa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan (wa kwanza kulia) akifunua jiwe la msingi kuashiria uzinduzi wa majengo ya SGR jijini Dar es Salaam, Agosti 2024.

# RAIS WA GUINEA BISSAU ATEMBELEA TRC NA KUJIONEA SHUGHULI ZA USAFIRISHAJI WA TRENI ZA SGR



Rais wa Guinea Bissau Mhe. Umaro Sissoco (kati) akiwa katika picha na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Januari Makamba (kulia) na Naibu Waziri wa Uchukuzi Mhe. David Kihenzile (kushoto) alipofanya ziara katika mradi wa SGR jijini Dar es Salaam Juni 2024.

**Na Mwandishi wetu.**

Rais wa Jamhuri ya Guinea Bissau Mhe. Umaro Sissoco Embalo atembelea Shirika la Reli Tanzania - TRC na kujionea ujenzi wa reli ya kiwango cha Kimataifa - SGR Juni, 2024.

Rais Embalo ambaye alikuwa nchini kwa ziara ya kikazi alitembelea Shirika la Reli Tanzania kujionea maendeleo na mafanikio katika sekta ya Uchukuzi ikiwemo ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa na shughuli za usafarishaji wa treni za SGR zilizoanza hivi karibuni.

Naibu Waziri wa Uchukuzi Mhe. David Kihenzile alisema kuwa ziara ya Rais Embalo nchini Tanzania inadhihirisha ni kwa namna gani ujenzi wa SGR umehamasisha nchi nyingi za Afrika kuwekeza katika sekta ya usafiri wa reli.

"Kuona Rais wa nchi anatoka nchi nyingine anakuja Tanzania kuona watanzania wamewezaje hilo ni jambo la kumshukuru Mungu na pili kumshukuru Rais wetu Mhe. Dkt.Samia Suluhu Hassan aliyetufikisha hapa" alisema Mhe. Kihenzile.

"Ujio wa Rais wa Guinea Bissau kwetu inamaanisha tunafanya kazi nzuri ambayo inapendwa na kuonekana na wenzetu kwahiyo tulipo ni pazuri, ni jambo la kujipongeza sisi watanzania" aliongeza Naibu Waziri.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kungu Kadogosa amesema kuwa ziara ya Rais wa Guinea Bissau itaongeza ushirikiano wa kibiashara baina ya Tanzania na Guinea Bissau kupitia ujenzi wa SGR.

" Tunashukuru sana ujio wa Rais wa Guinea Bissau, najua ni maamuzi ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Tanzania kumleta mgeni wake na sisi kama Taasisi na bodi yetu ni jambo la fahari ukizingatia yako mashirika zaidi ya 300 ya Serikali lakini Rais Embalo amechagua kuitembelea TRC" alisema Kadogosa.

Ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa utaleta hamasa katika sekta ya Biashara kati ya Tanzania na nchi za Afrika Mashariki na Jumuiya wa SADC kwa kuziunganisha nchi za Afrika kupitia usafiri wa uhakika na nafuu wa watu na bidhaa.

# VIONGOZI MBALIMBALI WASAFIRI NA TRENI YA MWENDOKASI



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango (kulia) akiwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Reli Tanzania - TRC Bwana Ally Karavina (kushoto) ndani ya treni ya mwendokasi inayotumia nishati ya umeme akisafiri kutoka Dodoma kuelekea jijini Dar es Salaam tarehe 4, Agosti 2024.



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango  akiwa ndani ya treni ya kisasa inayotumia nishati ya umeme akisafiri kutoka Dodoma kuelekea Dar es Salaam tarehe 4, Agosti 2024.



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akiwasili katika stesheni ya Dar es Salaam mara baada ya kusafiri kutoka Dodoma kuelekea Dar es Salaam kwa kutumia usafiri wa treni ya kisasa inayotumia nishati ya umeme tarehe 4, Agosti 2024.

# VIONGOZI MBALIMBALI WASAFIRI NA TRENI YA MWENDOKASI







Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa amesafiri kwa kutumia treni ya mwendokasi (SGR) kutokea Dodoma kwenda Dar es Salaam Agosti 30, 2024 ambapo alikuwa mgeni rasmi katika mkutano wa 12 wa Shirikisho la Watoa Huduma za Afya Afrika Mashariki uliofanyika katika kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam.

# TRC YAZINDUA KAMPENI YA UELEWA KUHUSU KUANZA HUDUMA ZA TRENI ZA SGR




Mkurugenzi Mkuu TRC Masanja Kadogosa (kulia) na Afisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB) Bwana Adam Mihayo wakikata utepe kuashiria uzinduzi rasmi wa kampeni ya RELI YETU katika stesheni ya SGR jijini Dar es Salaam, Juni 2024

**Na Mwandishi wetu.**

Shirika la Reli Tanzania lazindua kampeni ya uelewa kuhusu kuanza kwa huduma za safari za treni katika Reli ya kiwango cha Kimataifa - SGR kwenye hafla fupi iliyofanyika stesheni ya SGR Dar es Salaam, Juni 12, 2024.

Kampeni ina lengo la kuelimisha wananchi kuhusu matumizi ya huduma mpya za SGR pamoja na mambo muhimu ya kuzingatia katika masuala ya ulinzi na usalama wa abiria na mali zao ambapo kaulimbiu ya kampeni ni "TWENDE TUKAPANDE TRENI YETU, TUITUNZE, TUITHAMINI"

Mkurugenzi Mkuu Shirika la Reli Tanzania - TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa alisema kuwa katika utekelezaji wa maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha huduma za usafiri wa Treni zinaanza, Shirika la Reli Tanzania limeendelea kuchukua hatua kuhakikisha utekelezaji wa kuanza huduma za uendeshaji zinafanyika.

"Katika kutekeleza agizo la Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Shirika linautaarifu umma kuanza kwa utoaji huduma za awali za usafiri wa treni za SGR kati ya Dar es Salaam na Morogoro ifikapo Juni 14, 2024" alisema Kadogosa.

Aidha, Mkurugenzi Mkuu ameongeza kuwa kuanza kwa safari za treni za abiria kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro ni baada ya Shirika la Reli Tanzania kujiridhisha na utayari wa Miundombinu, Vitendea kazi (vichwa na Mabehewa) na mifumo ya Ishara na Mawasiliano.

"Shirika limefanya majaribio kadhaa kwa lengo la kujifunza na kukamilisha matakwa ya kisheria kuhakikisha vitendea kazi, njia na mifumo ya mawasiliano vimekidhi ufanisi na ubora kwaajili ya usalama wa abiria" alieleza Ndugu Kadogosa.

Sambamba na hilo Mkurugenzi Kadogosa aliwasihi wananchi kutumia huduma za usafiri wa treni kwani kupitia usafiri huo abiria wataweza kupata huduma zote ndani ya treni ikiwemo chakula, maliwato, mazingira mazuri ya kufanya kazi wakiwa safarini, huduma za mtandao pamoja na burudani.

Afisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB) Bwana Adam Mihayo alisema kuwa Benki ya Biashara Tanzania imeshirikiana bega kwa bega na Shirika la Reli Tanzania katika ujenzi wa mradi wa kimkakati wa SGR kuhakikisha mahitaji ya Watanzania yanatimia na kukuza uchumi wa nchi .

"Katika mradi huu wa kimkakati wa ujenzi wa SGR,

**Inaendelea uk. 8**

# TRC YAZINDUA KAMPENI YA UELEWA KUHUSU KUANZA HUDUMA ZA TRENI ZA SGR

**Inatoka Uk. 7**

TCB imeshirikiana na TRC katika maeneo ya kulipa wazabuni na ununuzi wa vichwa na mabehewa kutoka Ujerumani, hii imekuwa faraja Kwetu" alisema Bwana Mihayo.

Mihayo aliongeza kuwa "Tumeingia pia makubaliano na TRC ya ukusanyaji wa malipo kupitia ukataji tiketi, mfumo mzima utasimamiwa na TCB na makusanyo ya pesa taslimu pia yatasimamiwa na Benki yetu na kama TCB niwaahahidi Watanzania tutaendelea kutoa huduma bora kwa kushirikiana na TRC ili kutimiza matarajio ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania".

Afisa Biashara kutoka Shirika la Reli Tanzania Bi. Liliani Mselle amefafanua njia za ukataji tiketi za usafiri wa Treni za SGR kupitia njia ya mtandao na madirisha ya tiketi ndani ya stesheni za SGR. Shirika la Reli limeanisha aina na madaraja mbalimbali ya treni zitakazotumika katika usafirishaji wa awali ambapo kutakuwa na treni za kawaida ambazo zitasimama kila kituo kutoka Dar es Salaam – Morogoro na treni za mwendo wa haraka (express) ambazo zitatoka moja kwa moja bila kusimama kituo chochote kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro.

Kadhalika upande wa treni za mchongoko (EMU) zitakuwa na madaraja yafuatayo, Daraja la Juu (High Class), Daraja la Uchumi (Economy Class), Daraja la Biashara (Business Class) na Daraja la Kifalme la Biashara (Royal Business Class).



Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni ya uelewa kuhusu kuanza huduma za treni za SGR jijini Dar es Salaam Juni 2024.




Wahudumu wa treni ya SGR wakiwa wamebeba mabango yenye ujumbe tofauti wakati wa hafla ya uzinduzi wa kampeni ya RELI YETU katika stesheni ya Dar es Salaam, Juni 2024.

# TRC YAPOKEA SETI MBILI ZA TRENI YA EMU



Seti mbili za treni ya kisasa inayotumia nishati ya umeme - EMU (Electric Multiple Unit) zikiwa katika bandari ya Dar es Salaam zilipowasili Tanzania kutoka nchini Korea Kusini Juni 2024.

**Na Mwandishi wetu.**

Shirika la Reli Tanzania - TRC Ilimepokea Seti mbili (2) za treni ya kisasa inayotumia nishati ya umeme - EMU (Electric Multiple Unit) na vichwa nane (8) vya treni vya umeme kutoka nchini Korea ya Kusini Juni 2024..

Serikali kupitia TRC ilifanya manunuzi ya Seti kumi (10) za treni za EMU zinazotengenezwa na kampuni ya Hyundai Rotem ya nchini Korea Kusini, Seti moja ya EMU ina jumla ya mabehewa nane yakijumuisha kichwa kimoja mbele na kingine nyuma ikiwa na uwezo wa kubeba abiria 589 na kutembea kwa kasi ya kilomita 160 kwa saa.

Seti mbili (2) za EMU zinafikisha idadi ya seti tatu (Nyerere Express, Magufuli Express na Samia Express) zilizowasili nchini mpaka sasa, seti ya kwanza (Nyerere Express) iliyowasili mwezi Aprili 2024 inaendelea na majaribio.


Shirika la Reli Tanzania limeshapokea jumla ya mabehewa 65 ya abiria, vichwa 17 vya umeme na Seti tatu za EMU. Upokeaji wa vifaa vya uendeshaji vya reli ya kiwango cha SGR unaendelea kwa awamu tofauti, vifaa vipya vilivyowasili vitaendelea kufanyiwa majaribio kwaajili ya kujiridhisha kabla ya kuanza kutoa huduma.

Huduma za usafiri wa treni za abiria katika reli ya kiwango cha kimataifa - SGR zinaendelea kati ya Dar es Salaam na Morogoro ambapo jumla ya treni mbili (2) zinafanya safari nne (4) kila siku na kufanya jumla ya safari nane kwa siku.

Kuwasili kwa treni za EMU kunakwenda kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za usafiri katika reli ya kiwango cha kimataifa ambapo kuanzia Julai 25, 2024 TRC inatarajia kuanza huduma za usafiri kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma.



# WANANCHI WA MANISPAA TABORA NA IGALULA WILAYANI UYUI WANUFAIKA NA FIDIA KUTOKA TRC



**Na Mwandishi wetu.**

Shirika la Reli Tanzania - TRC limefanya malipo ya fidia Tabora Manispaa na Igalula wilaya ya Uyui mkoani Tabora kwa wananchi waliofanyiwa uthamini wa ardhi kwa ajili ya kupisha ujenzi wa njia kuu ya reli (Right of Way) na stesheni ya SGR Tabora katika kipande cha tatu cha ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa - SGR Makutupora - Tabora, Juni 2024.

Mhasibu kutoka TRC Hamad Hamad alisema takribani wananchi 383 wamelipwa fidia katika kitongoji cha Milembela, Timkeni kata ya Uyui - Tabora Manispaa na Igalula pia wengine wanaendelea kulipwa katika ofisi za kata.

"Malipo ya awamu hii yatafanyika pia katika vijiji vya Tambuka reli kata ya Nsololo,Kimungi kata ya Nsololo, Tura na Malongwe kata ya Kizengi wilayani Uyui mkoani Tabora, Shirika linahakikisha kila mwananchi aliyepisha ardhi kwa ajili ya kuwezesha ujenzi wa mradi anapata malipo kwa wakati" alieleza Hamad.

Afisa Miliki wa TRC Misango Mjandwa alisema wananchi ambao tayari wamelipwa stahiki zao kutokana na uthamini wa ardhi waliofanyiwa wanatakiwa kupisha ardhi zao kwa mujibu wa Sheria ili kumuwezesha mkandarasi kuendelea na shughuli za ujenzi wa mradi katika kipande cha tatu Makutupora - Tabora.

"Wananchi ambao hawajalipwa fidia zao tunaomba wawe watulivu wakati Shirika linakamilisha taratibu za malipo hayo kwa mujibu wa Sheria" alisisitiza Misango.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Milembela kata ya Uyui amepongeza zoezi la malipo kwa wananchi kwani zitawezesha ujenzi wa nyumba na ununuzi wa mashamba kwaajili ya kuendeleza shughuli za kilimo kama ilivyokua awali kabla ya uthamini kufanyika.

# MATUKIO MBALIMBALI KATIKA MAONESHO YA SABASABA 2024




Rais Mstaafu wa Tanzania Mhe. Dkt. Jakaya Kikwete (wa pili kushoto) akipata maelezo kutoka kwa Mhandisi Imani Mwandalima kuhusu mradi wa ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa alipotembelea banda la TRC katika maonesho ya SabaSaba jijini Dar es Salaam Julai 6, 2024.



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Bwana Habibu Suluo (kati) akisaini kitabu cha wageni alipotembelea banda la TRC SabaSaba jijini Dar es Salaam Julai 5, 2024.




Mtaalamu wa mawasiliano TRC Bwana Idala Ngalaba akitoa maelezo kuhusu mfumo wa mawasiliano unaotumika katika reli ya zamani kwa wageni waliotembelea banda la TRC katika maonesho ya SabaSaba jijini Dar es Salaam, Julai 2024.



Afisa Uhusiano TRC Augustino Bulegea akiwaelezea baadhi ya wageni waliotembelea banda la TRC kuhusu mfumo wa mawasiliano katika reli ya zamani (MGR) katika maonesho ya SabaSaba jijini Dar es Salaam, Julai 2024.




Afisa Uhusiano TRC Bi. Mwatime Ramadhani akiwaelezea baadhi ya wageni waliotembelea banda la TRC kuhusu mradi wa ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa katika maonesho ya SabaSaba jijini Dar es Salaam, Julai 2024.



Mgeni (kushoto) aliyetembelea banda la Shirika la Reli Tanzania akijaribu kifaa cha mawasilino kilichokuwa kikitumika katika uendesheji wa treni za MGR, katika maonesho ya SabaSaba jijini Dar es Salaam, Julai 2024.

# MAMBO YA KUZINGATIA UNAPOSAFIRI NA TRENI ZA MWENDOKASI


## UKOMO WA MIZIGO

**Biashara**




**Uchumi**




## VITU/VIFAA VISIVYORUHUSIWA



Mifuko ya Plastiki



Wanyama



Shangazi kaja na viroba



Silaha



Ndoo/Jaba



Chakula
Vinywaji



Vitu haramu/ madawa ya kulevya



Vilipuzi/Vitu vinavyolipuka



Kemikali hatari zenye sumu



Betri zenye asidi zinazoweza kuvuja



Vifaa vya mazoezi

**Maelezo zaidi piga 0800110042**



BODI YA WAHARIRI
MHARIRI MKUU | Jamila Mbarouk, MHARIRI MSAIDIZI/MSANIFU | Sami Omary
HABARI | Hemed Mohamed, Mariam Katunge MAKALA | Aziza Charles,  Amina Juma, Athumani Iddy
PICHA | Hassan Mbonde, Augustino Bulegea